# USAFIRI ARDHINI

Januari - Juni, 2024 ISSN 2961 - 6255 Toleo Na. 03

## LATRA YATANGAZA NAULI ZA ABIRIA WA DARAJA LA KAWAIDA TRENI YA SGR

Kwa mujibu wa Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA, amesema kuwa nauli hizo zimepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi LATRA kwa kuzingatia umbali wa kilomita baada ya kufanyia kazi maombi yaliyowasilishwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) na taarifa zilizopokelewa kutoka TRC na wadau wengine. Uk. 1

## MHE.MPOGOLO AWATUNUKU VYETI MADEREVA 1,518 WALIOTHIBITISHWA NA LATRA

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Mpogolo amewaambia madereva kuwa vyeti walivyotunukiwa vitatambulika kitaifa na kimataifa hasa kwa Nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC), Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) Uk. 14



## LATRA YAENDELEA KUBORESHA UDHIBITI WA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI NCHINI

"Katika kuboresha usimamizi wa VTS, Serikali imeandaa na kutangaza Kanuni za Matumizi ya VTS ya Mwaka 2024 ambazo zilianza kutumika mwezi Januari, 2024 ili kuimarisha Udhibiti na usalama kwa mabasi ya masafa marefu...." Uk. 23

# TAHARIRI



Karibu katika toleo la tatu la jarida la USAFIRI ARDHINI, Jarida hili limekusanya taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), ambayo yamefanyika kuanzia mwezi Januari hadi Juni 2024.

Kama ilivyo ada, jarida hili linaendelea kukuhabarisha kuhusu mambo mbalimbali, yanayotekelezwa na LATRA ikiwa ni sehemu ya utoaji wa elimu kuhusu shughuli za Mamlaka na masuala mbalimbali yanayogusa sekta ya Usafiri Ardhini nchini.

Mnamo Julai, 2024 Mamlaka imetangaza taarifa ya maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini kuhusu nauli za abiria wa daraja la kawaida kwa Treni ya Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora ambapo ilifuatiwa na kuanza rasmi kwa safari za SGR autoka Dar es Salaam hadi Morogoro.

Katika kipindi cha mwanzo wa mwaka 2024 Bodi ya Wakurugenzi Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imefanya ziara katika mradi wa Reli ya kisasa (SGR) na kukagua miundombinu pamoja na mabehewa ya reli hiyo, na Mamlaka kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRC) imefanikisha kwa kikubwa mradi wa reli hiyo ya kisasa ambao umezinduliwa rasmi Julai, 2024 kwa safari za Dar es Salaam kuelekea Morogoro na Dodoma.

AidhaMamlaka imeendelea kuboresha huduma za Usafiri Ardhini Nchini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa kufuatilia mwenendo wa mabasi na vichwa vya treni kupitia mfumo wa VTS na kuwasajili na kuwathibitisha madereva wa vyombo vinavyodhibitiwa kwa lengo la kuhakikisha usalama wa usafiri nchini unakuwepo ikiwa ni pamoja na kupunguza ajali nchini

Vilevile Wahudumu wa mabasi ya masafa marefu na mijini wameendelea kupatiwa elimu ili kusajiliwa ambapo wahudumu Kanda ya Kaskazini Tanzania Bara wamehitimu mafunzo yaliyotolewa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) pamoja na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kuanzia Februari 5-9, 2024 katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) ambapo wamejifunza masuala mbalimbali ikiwemo Sheria, Kanuni na Taratibu za LATRA.

Hayo ni baadhi tu kati ya mengi utakayosoma kwa kina katika jarida hili la USAFIRI ARDHINI. Nami nitumie fursa hii kukukaribisha tena katika kurasa hizi ili upate kufahamu vizuri huduma zinazotolewa na kufanyika katika sekta ya Usafiri Ardhini nchini kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini LATRA.

Nakutakia usomaji mwema.

# LATRA YATANGAZA NAULI ZA TRENI YA SGR KWA ABIRIA WA DARAJA LA KAWAIDA



Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetangaza taarifa ya maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini kuhusu nauli za abiria wa daraja la kawaida kwa Treni ya Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora.

Kwa mujibu wa Bw. Salum Pazzy, Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA alipotoa taarifa hiyo Juni 10, 2024 katika ofisini za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam, amesema kuwa nauli hizo zimepitishwa na Bodi ya Wakurugenzi LATRA kwa kuzingatia umbali wa kilomita. Kwa mfano, kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma ni kilomita 444.0 ambapo nauli yake ni TZs. 15,500/=, na pia zimepatikana baada ya kufanyia kazi maombi yaliyowasilishwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) na taarifa zilizopokelewa kutoka TRC na wadau wengine.

"Nauli hizi ni kwa daraja la kawaida kwa watu wazima na watoto kuanzia umri wa miaka 4 hadi 12 ambapo nauli zitalipwa na abiria kwa kilomita. Nauli itakayolipwa na mtu mzima na mtoto mwenye umri zaidi ya miaka 12 ni TZs. 69.51 kwa kilomita, na mtoto kuanzia miaka 4 hadi 12 atalipia TZs 34.76 kwa kilomita. Aidha mtoto mwenye umri chini ya miaka minne (4) hatalipa nauli, hata hivyo, taarifa zao na wasafiri wote zitatunzwa kwenye mfumo wa taarifa za abiria wanaosafiri kila siku," ameeleza Bw. Pazzy.

Vilevile amebainisha masharti ya kuzingatia kabla ya kuanza kutumika kwa nauli hizo kuwa ni mtoa huduma (TRC) kuwa na leseni ya usafirishaji, kuwa na ithibati ya usalama wa miundombinu ya reli na mabehewa, kutumia mfumo wa utoaji wa tiketi za kielekroni, kuunganisha mfumo wa tiketi za kieletroni na mifumo ya LATRA, kukokotoa malipo na utunzaji taarifa za abiria, nauli iliyolipwa, tiketi za kielektroni zilizotolewa, kodi za Serikali na tozo za kisheria na kuwa na watumishi wa kada muhimu kwa masuala ya ufundi na uendeshaji wa treni ya SGR ikiwa ni pamoja na madereva waliothibitishwa na wahudumu waliosajiliwa na LATRA.

Pia, Bw. Pazzy amesema kuwa, maeneo ya msingi ya kuzingatiwa na mtoa huduma ni pamoja na kuweka mfumo wa usimamizi wa utoaji taarifa kwa wasafiri na mfumo wa ufuatiliaji wa mwenendo wa

>>>Inaendelea Uk. 2

> **"Nauli hizi ni kwa daraja la kawaida kwa watu wazima na watoto kuanzia umri wa miaka 4 hadi 12 ambapo nauli zitalipwa na abiria kwa kilomita."**
>
> *Bw. Salum Pazzy*

>>>Inatoka Uk. 1

## LATRA YATANGAZA NAULI ZA ABIRIA WA DARAJA LA KAWAIDA TRENI YA SGR

treni, kuweka nauli za safari ya kituo kwa kituo katika maeneo yanayoonekana na abiria kiurahisi kwa wakati wote, kuhakikisha uwepo wa huduma bora kwa wateja ikiwemo mazingira ya vituo (stesheni), usafi wa mabehewa, chakula na vinywaji, maji safi na salama, mwanga wa kutosha, na kuweka utaratibu wa fidia dhidi ya majanga na upotevu wa mizigo ya abiria na kuzingatia vigezo vya usalama wa mabehewa na miundombinu ya reli kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na

## MAGOMBANA: MAONI YENU NI MUHIMU ILI KUBORESHA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI NCHINI

Wadau wa usafiri ardhini wamesisitizwa kutoa maoni yao kuhusu Sheria ya Leseni za Usafirishaji Sura ya 317, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 na Kanuni zake, ili kuboresha huduma za usafiri ardhini nchini.

Hayo yameelezwa na Bw. Andrew Magombana, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Usafiri kwa Njia ya Barabara kutoka Wizara ya Uchukuzi aliyemuwakilisha Prof. Godius Kahyarara, Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, katika kikao cha wadau cha kupokea maoni kuhusu maboresho ya Sheria ya Leseni za Usafirishaji Sura ya 317, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura 413 na Kanuni zake, kilichofanyika Juni 05, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa Arnaoutouglou, Jijini Dar es Salaam.

Bw. Magombana amezitaja kanuni hizo kuwa ni Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Huduma ya Kukodi) za Mwaka 2020, Kanuni za Leseni (Huduma za Usafiri wa Umma) za Mwaka 2020, Kanuni za Leseni (Vyombo vya kubeba mizigo) za Mwaka 2020, Kanuni za Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko za Mamlaka ya Udhibiti

>>>Inaendelea Uk. 3




*Bw. Andrew Magombana, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Usafiri kwa Njia ya Barabara kutoka Wizara ya Uchukuzi akizungumza na wadau mbalimbali wa Usafiri Ardhini waliojitokeza kutoa maoni yao kuhusu Sheria ya Leseni za Usafirishaji Sura ya 317, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 na Kanuni zake, Juni 05, 2024 ,Ukumbi wa Mikutano Arnaoutouglou*

>>>Inatoka Uk. 3

## MAGOMBANA: MAONI YENU NI MUHIMU ILI KUBORESHA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI NCHINI

Usafiri Ardhini za Mwaka 2024, pamoja na Kanuni za Vigezo na Masharti ya Kutoa Huduma zinazodhibitiwa za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024.

"Kwa maoni yenu, tunaweza kupata maboresho ya Sheria na Kanuni ambayo yatasaidia shughuli za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na kuleta matokeo chanya kwa nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuwa na huduma za usafiri zilizo salama, za uhakika na rafiki kwa mazingira," amesisitiza Bw. Magombana.

Naye CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amesema kuwa, Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasisitiza suala la ushirikishaji wa wadau ambalo limekuwa likitekelezwa kwa vitendo na Wizara ya Uchukuzi na LATRA ndio maana mkutano umeandaliwa na wadau wameshirikishwa na kuwa huru kutoa maoni yao ambayo yatafanyiwa kazi.

Vilevile ameeleza kuwa, LATRA inashirikiana vizuri na wadau wake, pia Wizara ya Uchukuzi na Mamlaka wanataka kuwa na Sheria rafiki inayowajali na itakayosaidia kukuza mitaji ya wasafirishaji ili waweze kutekeleza shughuli zao za kuwahudumia wananchi kupitia usafirishaji, "tunachokifanya leo, si mwisho na tutakuwa na nafasi ya kukutana na kufanya maboresho ya Sheria na Kanuni zetu mara kwa mara ili kuwa na sekta ya usafirishaji yenye tija na manufaa kwa wananchi, wasafirishaji na Serikali kwa jumla."

> **"Tunachokifanya leo, si mwisho na tutakuwa na nafasi ya kukutana na kufanya maboresho ya Sheria na Kanuni zetu mara kwa mara"**
>
> *CPA Habibu Suluo*

Pia, CPA Suluo amesema wadau hao na wale ambao hawakuweza kufika katika mkutano huo, waendelee kutuma maoni yao kwa maandishi kupitia baruapepe ya group.maoni@latra.go.tz mpaka tarehe 12 Juni, 2024.

Naye Bi. Mwadawa Sultan, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria kutoka LATRA amesema sababu za kufanya maboresho ya Sheria ambazo ni kufuta baadhi ya majukumu ambayo hayatekelezeki kwa Mamlaka kwa kuwa yanaratibiwa na Taasisi nyingine za Serikali, kutoa tafsiri ya maneno mbalimbali ambayo yalikuwa hayana tafsiri mahsusi, kutambulisha Mawakala wa Mamlaka katika Sheria zote mbili na Kanuni zote chini ya Sheria za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini na kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya vifungu mfano kufafanua ni mazingira gani yanaweza kupelekea mgongano wa maslahi,

Pia, Bi. Mwadawa amesema sababu nyingine ni kufuta utaratibu wa zamani wa utoaji wa leseni uliotolewa chini ya Sheria ya leseni (Transport licencing Act Cap 317) ambao ulikuwa chini ya mamlaka za Uteuzi (appointing Authorities) na kuweka wa sasa ambao upo chini ya Mamlaka ya leseni (Licencing authority) ambayo ni LATRA, kuendana na uhalisia wa mazingira yalivyo sasa kutokana na ukuaji wa teknolojia na gharama za uendeshaji kwa ujumla pamoja na kuweka bayana muda kukata rufaa kwa ambaye hajaridhika na maamuzi ya Bodi kwenda katika Baraza la Ushindani ndani ya siku 14, ambapo kwa sasa Sheria ya LATRA haijataja muda.

>>>Inaendelea Uk. 4

>>>Inatoka Uk. 3

## MAGOMBANA: MAONI YENU NI MUHIMU ILI KUBORESHA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI NCHINI

Vilevile Bi. Mwadawa ameainisha sababu za kufanya maboresho ya Kanuni kuwa ni viwango vilivyopo ni vya muda mrefu haviendani na hali halisi ya mabadiliko ya uchumi na biashara, kutenganisha kati ya huduma za mabasi ya abiria kwa umma na huduma za vyombo vya kukodi, kutenganisha adhabu kwa vyombo vya usafiri kulingana na uwezo wa chombo husika mfano malori makubwa na vyombo vidogo vya kubeba mizigo kama vile pikipiki za magurudumu matatu (guta)

Ameongeza kuwa, sababu nyingine ni kutambua Kanuni zilizotengenezwa kwa ajili ya Ufifilishaji wa Makosa na adhabu ili zitumike ipasavyo na kupendekeza kufutwa kwa kanuni zinazobainisha ufifilishaji wa makosa kwenye Kanuni hizi, Kwa Kanuni za mwaka 2024, sababu kubwa ni utekelezaji wa maoni ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Sheria ndogo.

Wadau mbalimbali waliohudhuria mkutano huo wameipongeza Wizara ya Uchukuzi na LATRA kwa jitihada za dhati za kuboresha

## WAWILI MBARONI KWA KUKIUKA MASHARTI YA LESENI




*CPA Habibu Suluo Mkurugenzi Mkuu wa LATRA pamoja na SACP Ramadhani Ng'anzi, Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wakikagua tiketi za abiria zitolewazo na kampuni ya Kilimanjaro Express.*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani imewatia mbaroni wasimamizi wawili wa kampuni ya usafirishaji Kilimanjaro Express kwa kosa la kukiuka masharti ya leseni ikiwemo kuzidisha nauli kuliko kiwango kilichopangwa na Mamlaka pamoja na kutotoa tiketi za kielekroni

Akizungumza na abiria baada ya ukaguzi wa kushtukiza uliofanywa na LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kote nchini, CPA Habibu Suluo Mkurugenzi Mkuu wa LATRA amesema kuwa Mamlaka imefikia hatua hiyo baada kampuni hiyo kufanya makosa hayo kwa kujirudia bila kubadilika.

"Disemba 22, 2023 timu ya ukaguzi tulipita hapa usiku na kukuta abiria wametozwa TZS. 44,000/= badala ya TZS. 42,000/= iliyoidhinishwa, pia walikuwa hawatoi tiketi za kielektroni, tuliwaonya na kuwaamuru wawarudishie abiria kiasi kilichozidi na wakafanya hivyo, lakini leo tukiwa kwenye ukaguzi wa kushtukiza tumebaini wakiendelea na makosa yaleyale ndio maana kwanza tumewapeleka Polisi na mpaka kufikia Jumatatu Januari 8, 2024 hawatasafirisha abiria kama watakuwa hawajaanza kutumia tiketi za kielektroni," amesema CPA. Suluo.

Aidha, CPA Suluo amewahimiza wamiliki wa shule zenye mabasi ya shule

>>>Inaendelea Uk. 5

>>>Inatoka Uk. 4

# WAWILI MBARONI KWA KUKIUKA MASHARTI YA LESENI

kuhakikisha leseni zao ni hai na magari yao ni salama kabla ya kufungua shule ili kuhakikisha usalama wa safari na wanafunzi kwa jumla.

"Magari ya Shule yanapewa leseni na LATRA baada ya kukaguliwa kwa kina na Jeshi la Polisi, ndio maana unaweza kuona hakuna matukio mabaya ya magari ya shule kwa upande wa ajali zaidi ya lile la Mtwara na lenyewe lilikuwa halijakaguliwa, kwahiyo niwahimize wamiliki wa shule kabla ya jumatatu ambapo shule zinafunguliwa magari yao yawe yamekaguliwa na yana leseni hai ya LATRA, sisi tutapita mitaani kufanya ukaguzi, hivyo ili kuepusha usumbufu usio wa lazima tufuate matakwa ya Kisheria," ameongeza CPA Suluo.

Kwa upande wake, SACP Ramadhani Ng'anzi, Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani amewataka wasafirishaji kufuata matakwa ya Kisheria ikiwa ni pamoja na masharti ya leseni zao sambamba na wamiliki wa Shule kuhakikisha magari yao yanakaguliwa ili kuboresha huduma za usafiri nchini.

"Tunapokea taarifa kutoka kwa raia wema kuhusu wasafirishaji wanaokiuka masharti ya leseni, mfano mzuri ni hii kampuni ya Kilimanjaro ambayo katika ukaguzi wetu tumebaini anazidisha nauli ndiyo maana msimamizi wa kituo hiki na msaidizi wake tumewaweka chini ya ulinzi, hivyo nitoe wito kwa wasafirishaji kufuata Sheria za nchi ili kuepuka usumbufu usio wa lazima, na wamiliki wa shule ni vyema kufuata Sheria ambazo zinatuongoza sisi sote ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wana magari mazima, salama na yaliyokaguliwa na kutoruhusu aina yoyote ya burudani," amesema SACP Ng'anzi.

> **"Nimefurahi sana mmekuja hapa kutusaidia, kiukweli sisi wananchi tulikuwa tunanyanyasika sana"**
>
> ***Bi. Pendo Dosta***

Naye Bi. Pendo Dosta, abiria aliyezidishiwa nauli ameishukuru Mamlaka kwa kazi nzuri inayoifanya hasa ya kutetea abiria ambapo yeye alirejeshewa nauli yake katika ukaguzi huo, pia ameipongeza Mamlaka na Jeshi la Polisi kwa kuendesha zoezi hilo kwa weledi na ufanisi.

"Nimefurahi sana mmekuja hapa kutusaidia, kiukweli sisi wananchi tulikuwa tunanyanyasika sana, na tulikuwa hatuna budi kulipa kiasi kilichozidi kwa sababu tulikuwa hatujui nini cha kufanya na tunaitaka safari, mimi namshukuru sana Rais wetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine wote, kwa hili la leo nimeamini kuwa wanatuona na wanatusaidia," amesema Bi. Pendo.

Kufuatia ukaguzi wa kushtukiza uliofanywa na LATRA pamoja na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani na kubaini kutobadilika na kujirudia kwa makosa kwa kampuni ya Kilimanjaro Express yenye mabasi 35, LATRA imeifungia kutoa huduma ya usafiri kampuni hiyo kuanzia Jumatatu Januari 8, 2024 mpaka pale itakapoonesha utayari wa kufuata masharti ya Leseni kwa mujibu wa Sheria.

Mabasi 35 ya Kampuni ya Kilimanjaro Express yaliyofungiwa ni T165DMH, T491ARB, T772ADJ, T830AXR, T676DHY, T805DDB, T689DHY, T893APD, T814BGZ, T545BHY, T639AQN, T278ALQ, T860BVA, T708DGQ, T163DMH, T540AQK, T675DHY, T705DGQ, T855AXR, T804DDB, T895APD, T709DGQ, T622DPT, T983AWY, T904ACN, T546BHY, T178EAU, T176EAU, T173EAU, T177EAU, T832ASM, T434DKL, T809BGZ,

# AGIZO LA MHE. RAIS, LAWAKUTANISHA BODI YA WAKURUGENZI NA MENEJIMENTI YA LATRA NA TRC



*Prof. Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya LATRA (Kushoto) na Bw. Ally Karama Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC wakifuatilia kwa umakini wasilisho lililoandaliwa na TRC wakati wa ziara ya Bodi ya LATRA katika mradi wa Reli ya kisasa (SGR)*

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imefanya ziara katika mradi wa Reli ya kisasa (SGR) na kukagua miundombinu pamoja na mabehewa ya reli hiyo, ziara hiyo imefuatiwa baada ya tamko la Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri wa Muungano Tanzania ambaye ameagiza mpaka Julai, 2024 huduma ya reli hiyo ianze kutolewa.

Akizungumza katika ziara hiyo Prof. Ahmed Mohamed Ame ameeleza kuwa LATRA inajukumu kubwa la kusimamia reli na miundombinu yake ikiwa ni pamoja na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na Shirika la Reli nchini (TRC).

"Kilichofanyika ni kitu kikubwa kwa sababu tumeweza kutengeneza mpango kazi na tumezitaka menejimenti zetu mpango kazi uanze kutekelezwa kimoja baada ya kingine kwa muda maalum na hadi kufikia mwezi mei mambo yote tuliyokubaliana yawe yametimia na ikiwezekana huduma zianze hapo hapo na sio lazima kusubiri mpaka mwezi Julai" ameeleza Prof. Ame.

> **"Tumeweza kutengeneza mpango kazi na tumezitaka menejimenti zetu mpango kazi uanze kutekelezwa kimoja baada ya kingine**
>
> *Prof. Ahmed Ame*

Kwa upande wake Bw. Ally Karama Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC amesema ugeni wa leo ulikuwa na lengo la kukagua Reli ya kisasa (SGR) kujua imefikia wapi na inaelekea wapi, katika majadiliano hayo wametoa ukomo wa muda mpaka kufika mwezi Mei mwaka huu vifaa vyote na taratibu muhimu za kuwezesha mradi ziwe zimeshatimia tayari kwa kuanza kazi.

"Malengo tuliojiwekea kama bodi ni kuhakikisha kwamba mpaka mwezi mei tuwe na uwezo wa kuanza kazi na sio kungoja mpaka siku iliyowekwa na Mhe.Dkt Samia, tunafahamu LATRA kama mamlaka inayodhibiti usafiri wa reli lazima watupe vyeti ili kutuwezesha kuanza kazi na kuweka njia yetu kuwa wazi na tunaamini chochote kikitokea watatupa ushirikiano kama tukifuata taratibu zote kuanzia sasa mpaka tutakapo anza kutoa huduma kwenda Dodoma Bw. Ally Karama ameeleza.

Naye CPA Habibu Suluo Mkurugenzi mkuu wa

>>>Inaendelea Uk. 7

>>>Inatoka Uk. 6

## AGIZO LA MHE. RAIS, LAWAKUTANISHA BODI YA WAKURUGENZI...

LATRA ameipongeza bodi ya wakurugenzi na menejimenti ya TRC kwa kusimamia mradi mkubwa wenye manufaa makubwa kwa nchi na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ujumla lakini pia ameipongeza serikali ya awamu ya sita kwa uwekezaji huo wa kipekee.

"Watanzania watafurahia uwekezaji huu na sisi LATRA jukumu letu ni kuhakikisha usalama na ubora, mpaka sasa hivi haya mabehewa tumeshayakagua tumeona yako katika ubora wa kuanza kutumika, njia tumekagua lakini kuna maeneo yanahitaji kumalizika na kuwekewa fensi kwa sababu hii njia lazima iwe na fensi ya kuwezesha sehemu ambayo reli zinapishana na hilo linafanyika na tunatarajia maeneo ambayo hayajakamilika mpaka mwezi wa tano yatakuwa yamekamilika" ameeleza CPA Suluo.

Aidha CPA Suluo ameongeza kuwa Mamlaka inahakikisha ubora wa kiuchumi na ubora wa kiusalama kwahio niwatake wananchi tushirikiane kulinda miundombinu hii kwa sababu uwekezaji huu ni mkubwa sana kwahio tunaomba tutunze rasilimali hii na tuwe walinzi.

Naye Bw. Senzige Kisenge Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TRC akiongelea ziara ya bodi ya wakurugenzi na menejimenti ya LATRA kuwa wamejipanga na wapo tayari kutekeleza maagizo ya bodi hiyo.

"Ninachoweza kusema ni kwamba maandalizi yanaendelea vizuri mambo mengi ya kiufundi yamekamilika kwa kiasi kikubwa lakini kabla hujaanza kutoa huduma ili kulinda usalama lazima tufanye majaribio mengi sana na saivi tupo katika hatua za kufanya majaribio ya njia yenyewe na mabehewa, tukishamaliza mamlaka itakuja kuthibitisha na kutupa vyeti na ninachoweza kuwaambia



*Wajumbe wa Bodi ya LATRA wakiongozwa na Prof. Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Menejimenti na wafanyakazi wa LATRA wakiongozwa na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA wakikagua miundombinu ya Reli wakati wa ziara ya Bodi ya LATRA katika mradi wa Reli ya kisasa (SGR)*

# LATRA YAWANOA WANAHABARI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imewaasa wanahabari kutumia kalamu zao vizuri ili kuleta mabadiliko katika jamii kwani Mamlaka inaamini nguvu ya kalamu zao inaweza kusaidia kujenga Taifa linalozingatia utu, uadilifu amani na utulivu.

Hayo yamesemwa na Wakili Tumaini Silaa, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi ya LATRA wakati akifungua semina ya siku mbili ili kuwajengea uwezo Wanahabari Mabalozi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuhusu kazi na majukumu ya LATRA katika ukumbi wa hoteli ya Njuweni - Kibaha Mkoani Pwani kuanzia Februari 26 hadi 27, 2024.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa semina hiyo Wakili Silaa amewasihi mabalozi hao kuzingatia uzalendo katika utendaji wa kazi zao pamoja na kuzingatia maadili kwani kufanya hivyo kutaleta maendeleo chanya kwa taifa na sekta ya usafiri kwa jumla.

"Tunatambua umuhimu wenu na kazi kubwa mnayofanya kwa LATRA na kwa nchi hii, vilevile tunatambua mchango mkubwa ambao mmeufanya kwetu katika kuhabarisha na kutoa elimu kwa umma kuhusu mambo mbalimbali yanayofanywa na Mamlaka, niwasihi muendelee kufanya kazi kwa kutanguliza uzalendo mbele kwa sababu na ninyi pia mnaishi katika nchi hii, na mzitumie vyema kalamu zenu katika kuuhabarisha umma," amesema Wakili Silaa.

Kwa upande wake CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu LATRA amewapongeza wanahabari mabalozi hao kwa kuhudhuria semina hiyo pamoja kuwa ni mara ya kwanza LATRA kuandaa semina kama hiyo na kuongeza kuwa LATRA inathamini sana kazi yao ya

>>>**Inaendelea Uk. 9**



*Mha. Hanya Mbawala, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Reli (aliyesimama) akielezea majukumu ya LATRA katika udhibiti wa Usafiri wa Reli kwa wanahabari waliohudhuria semina ya siku mbili ili kuwajengea uwezo Wanahabari Mabalozi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Februari 26 hadi 27, 2024, ukumbi wa hoteli ya Njuweni - Kibaha - Pwani*




*Wakili Tumaini Silaa, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi ya LATRA akifungua semina ya siku mbili ili kuwajengea uwezo Wanahabari Mabalozi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Februari 26 hadi 27, 2024, ukumbi wa hoteli ya Njuweni, Kibaha - Pwani*

>>>**Inatoka Uk. 8**

## LATRA YAWANOA WANAHABARI

kuhabarisha jamii kuhusiana na majukumu mbalimbali ya Mamlaka.

"Niwashukuru sana kwa kukubali mwaliko wetu na kuja kuhudhuria semina hii, naamini mahali ambapo wanahabari wapo wananchi huwakilishwa vyema, ni matarajio yetu kuwa uwepo wenu hapa utawezesha kujifunza na kuufikishia umma wa watanzania taarifa sahihi kuhusu juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia LATRA ili kujenga Taifa bora lenye kuchapa kazi kwa weledi, amani, utulivu, umoja, mshikamano na upendo miongoni mwa watanzania," amesema CPA Suluo.

Aidha, CPA Suluo ameeleza kuwa, mafanikio ambayo LATRA imeyapata ni kutokana na juhudi za makusudi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia kwa kuijengea LATRA mazingira bora na mazuri katika kusimamia sekta ya usafiri ardhini kwa weledi na ufanisi mkubwa.

"Natumia fursa hii kutoa Pongezi za dhati kwa Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri wenye mafanikio mengi makubwa katika Awamu hii ya Sita. Kwa uchache niseme uongozi wa Mhe. Dkt Samia umetujengea mazingira mazuri, bora na rafiki ya kusimamia sekta ya usafiri ardhini kwa weledi na ufanisi mkubwa tukizingatia sana ushirikishwaji wa wadau wetu wote muhimu" amesema CPA Suluo.

Naye Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara amewaasa mabalozi hao wa habari kushirikiana kuelimisha umma kuhusu haki na wajibu wao watumiapo vyombo vya moto kibiashara pamoja na kuzitolea taarifa changamoto za usafiri zinazowakabili wananchi kwa LATRA kwani kufanya hivyo italeta tija katika kuboresha sekta ya Usafiri Ardhini.

Kwa upande wake Bi. Helen Nachilongo, mwandishi wa gazeti la The Citizen ameishukuru LATRA kwa kuwapatia nafasi ya kushiriki katika semina ya kuwajengea uwezo na kuiomba Mamlaka iendelee na utaratibu huo wa kuwapatia mafunzo kwani imeweka alama kubwa kwao.

Naye Bw. Saidi Mohammed, mwandishi wa Clouds FM amewasihi mabalozi wenzake kuwanufaisha wananchi kwa kile walichokipata kutoka LATRA kwani ni jukumu lao kama waandishi.

Wataalamu wa LATRA waliwasilisha mada mbalimbali kwenye semina hiyo ikiwemo Kanuni Mpya za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za mwaka 2024 zinazosimamia matumizi ya mfumo wa Tiketi Mtandao, Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari, Kanuni za Uwezeshaji wa Watoa Huduma za Usafirishaji, kanuni za Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko,

# LATRA YATUNUKIWA CHETI NA TAT




*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi MKuu wa LATRA akisoma Cheti ambacho LATRA imetunukiwa na Chama cha Wasafirishaji Tanzania (TAT) Machi 7, 2024 katika Ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.*

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amepokea cheti cha kutambua na kuthamini mchango wa Mamlaka katika maendeleo ya sekta ya usafiri nchini kutoka kwa Chama cha Wasafirishaji Tanzania (TAT). Machi 7, 2024 katika Ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa cheti hicho, CPA Suluo amesema cheti alichopokea ni kielelezo tosha cha utumishi uliotukuka wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa ndiye aliyeweka mazingira bora, rafiki na wezeshi yaliyochagiza kukua na kuboreshwa kwa sekta ya usafiri nchini.

"Anayestahili hili ni Mhe. Rais Samia ambaye aliniteua ili nimsaidie kusimamia sekta hii. Niwaombe muendelee kuchapa kazi kwa bidii kwa kuwa ndio njia pekee ya kumshukuru kwa kazi kubwa na nzuri anayoendelea kuifanya kwa wananchi na Taifa kwa jumla," ameeleza CPA Suluo.

Vilevile amesema kuwa, Serikali inatambua na inathamini kazi kubwa inayofanywa na TAT na vyama vingine vya wasafirishaji na pia inatambua mchango wao katika uchumi wa nchi, na Mamlaka itaendelea kushirikiana nao katika kila hatua ili kufikia malengo na maono ya Mhe. Rais Samia ya kuifanya sekta ya usafiri kuwa bora zaidi.

Pia ameeleza kuwa, cheti hicho kimeipa Mamlaka changamoto zaidi ya kuongeza umakini na ufanisi wakati wa kutekeleza majukumu ya kiudhibiti.

Akizungumza kwa niaba ya wanachama wa TAT, Bw. Omar Kiponza, Makamu wa Rais TAT amesema kuwa, wao kama wadau wa usafirishaji nchini, wanatambua juhudi na kazi kubwa inayofanywa na LATRA katika kuhakikisha sekta ya usafiri ardhini inakuwa bora na salama.

Aidha, Bw. Kiponza amempongeza CPA Suluo na uongozi wa Mamlaka kwa kusimamia sekta ya usafiri ardhini kwa weledi na ufanisi, pia kwa kuwa wasikivu na kutatua changamoto zao kwa wakati.

# MHE. CHALAMILA: FUATENI SHERIA ZA NCHI, MFANYE BIASHARA KWA UHURU



*Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam akiendesha kikao kati ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dar es salaam, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani pamoja na Mmiliki wa kampuni ya Kilimanjaro Express, ili kujadili kufungiwa kwa kampuni hiyo Januari 8, 2023 Ofisi za LATRA Dar es Salaam.*

Mhe. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam amewataka wasafirishaji kufuata Sheria za nchi ikiwa ni pamoja na Sheria za Usalama Barabarani na Masharti ya Leseni zao ili kuboresha huduma za usafiri nchini na kuepusha migogoro na Mamlaka za Serikali zinazosimamia Sheria hizo.

Mhe. Chalamila ameyasema hayo kwenye kikao kati ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dar es salaam, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani pamoja na Mmiliki wa kampuni ya Kilimanjaro Express, ili kujadili kufungiwa kwa kampuni hiyo Januari 8, 2023 Ofisi za LATRA Dar es Salaam.

Akizungumza katika kikao hicho, Mhe. Chalamila amemhimiza Mmiliki wa kampuni ya Kilimanjaro Express kufuata maagizo aliyopewa katika barua ya kufungiwa kutoa huduma ili kumuwezesha kufunguliwa na kuendelea kutoa huduma.

"Tumeweka Mfumo wa Tiketi Mtandao lakini bado kuna baadhi yenu mnakaidi, kwa kufanya hivi mazingira yenu ya kufanya kazi yatakuwa magumu mno, kuleta barua kwa Mamlaka na kuanza kufanya kazi wakati bado hamjaridhiwa na Mamlaka ni kiburi. Niwaombe msome kwa umakini kipengele cha nne cha barua yenu na mkitekeleze kama kilivyo ili muweze kuruhusiwa kutoa huduma," amesema Mhe. Chalamila.

Aidha, Mhe Chalamila amezihimiza Mamlaka zinazosimamia Sheria kufanya kazi kikamilifu na kuwaasa wasafirishaji wote kufuata Sheria za nchi badala ya kutegemea uhusiano walionao na watu walio na nafasi mbalimbali katika jamii, ili kuweka jamii yenye ustawi bora na endelevu.

"Kwanza niwapongeze kwa hili na niwaombe tuendelee kuwa wakali kwani litakapoharibika jambo macho yote yatakuwa kwetu, namshukuru Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliona

> **"Unaweza kufahamiana na mtu aliye madarakani leo akakusaidia lakini kesho hayupo madarakani na Sheria bado ipo, hivyo ni vyema kutii Sheria"**
>
> *• Mhe. Albert Chalamila*

suala la safari za saa 24, hii ni fursa nzuri hivyo muitumie kwa kutii Sheria, unaweza kufahamiana na mtu aliye madarakani leo akakusaidia lakini kesho hayupo madarakani na Sheria bado ipo, hivyo ni vyema kutii Sheria," amesema Mhe. Chalamila.

Kwa upande wake CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi

>>>Inaendelea Uk. 12

>>>Inatoka Uk. 11

## MHE. CHALAMILA: FUATENI SHERIA ZA NCHI....

Mkuu wa LATRA ameelezea hatua ambazo Mamlaka imezichukua kabla ya kuichukulia hatua kampuni hiyo ya Kilimanjaro Express.

"Disemba 22, 2023 tulifanya ukaguzi usiku na moja ya sehemu tuliyopita ni ofisi ya Kilimanjaro Express, tulikuta abiria wamezidishiwa nauli, tuliamuru kiasi kilichozidi kirudishwe na wakafanya hivyo, pia tuliwasiliana na kituo cha Taifa cha Kutunza Data Kimtandao (NIDC) na wakatueleza kuwa mtoa huduma huyu alikwenda kwa ajili ya kufanya majaribio ya kutumia Mfumo wa Tiketi Mtandao na si kuanza kutumia, hivyo Januari 6, 2024 tukiwa kwenye ukaguzi tukapita katika ofisi yao na kukuta wamewazidishia tena nauli abiria na hawatoi Tiketi za Kielekroni, hivyo tukaamua kuchuka hatua kwa mujibu wa Sheria," amesema CPA Suluo.

Naye SACP Ramadhani Ng'anzi, kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani amewaasa wasafirishaji wote kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa ili huduma inayotolewa iwe bora na yenye kugusa maslahi ya pande zote wasafirishaji, abiria na Serikali.

"Kilimanjaro Express kama wasafirishaji wengine anapaswa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa, Serikali inategemea sekta binafsi kwenye usafirishaji lakini haimaanishi wasafirishaji wapo juu ya Sheria, ndiyo maana hata leo asubuhi tumezuia abiria wapya kukatishwa tiketi, wanafunzi na wazazi waliokuwa na wekesho la safari ikafanyika busara ya kuwasafirisha kwa kibali maalumu, na huo ndio msimamo wetu," amesema SACP ng'anzi.

Wakili Dickson Ngowi ni mwanasheria wa kampuni ya Kilimanjaro Express, na anakubali kutendeka kwa makosa na kuahidi kutojirudia huku maelekezo ya mwanzo ya Mamlaka yakiwa yamefanyiwa kazi.

"Aliyoyasema Mkurugenzi wa LATRA ni sahihi, tumekubali kuwa kuna makosa yametokea na ni makosa ya kibinadamu, hivyo kwa niaba ya Kilimanjaro Express napenda kuomba radhi kwa Serikali na wananchi ambao tunawahudumia na tunaahidi kuwa haitajirudia tena," amesema Wakili Ngowi.

Januari 6, 2024, LATRA ilifanya ukaguzi wa kushtukiza katika Kituo Kikuu cha Mabasi Magufuli na ofisi ya Kilimanjaro Express ili kukagua hali ya usafiri na utekelezaji wa masharti ya leseni. Katika ukaguzi huo Mamlaka ilibaini kampuni ya Kilimanjaro Express kuwa na makosa kadhaa, ikiwemo kutoza nauli kubwa kuliko iliyoidhinishwa na Mamlaka na kutotoa tiketi za kielekroni likiwa ni kosa la kujirudia, hii ikasababisha kampuni hiyo kufungiwa kuanzia Januari 8, 2024 mpaka watakapotimiza vigezo walivyowekewa.

Vigezo ambavyo kampuni hiyo imepewa ni pamoja na kuanza kutumia mfumo wa Tiketi Mtandao ulioidhinishwa na Mamlaka, kuingiza





## GHARAMA ZA LESENI

vyombo vinavyodhibitiwa na **LATRA** kwa mwaka

| Aina ya Chombo | | Aina ya Leseni | | Gharama |
|---|---|---|---|---|
| | Pikipiki ya magurudumu Mawili | Kawaida | D1 | Tsh 17,000/= |
| | | Taksi Mtandao | D4 | Tsh 35,000/= |
| | Pikipiki ya magurudumu Matatu | Kawaida | D2 | Tsh 22,000/= |
| | | Taksi Mtandao | D4 | Tsh 35,000/= |
| | Taksi | Kawaida | D3 | Tsh 35,000/= |
| | | Taksi Mtandao | D4 | Tsh 35,000/= |
| | Magari Maalum ya Kukodi | SPECIAL HIRE | D6 | Tsh 310,000/= |

NB:
Gharama hizi zinajumuisha gharama ya maombi ya Leseni Tsh 2,000/=kwa pikipiki za magurudumu mawili na matatu (kawaida) na Tsh 10,000/= kwa leseni nyingine.

www.latra.go.tz 0800 11 00 19 0800 11 00 20



## GHARAMA ZA LESENI

Mabasi ya mjini (Daladala) kwa mwaka

| Idadi ya Abiria | Leseni | Gharama |
|---|---|---|
| 1 - 15 | A1 | Tsh 45,000/= |
| 16 - 25 | A2 | Tsh 60,000/= |
| 26 - 45 | A3 | Tsh 100,000/= |
| 45 - 65 | A4 | Tsh 110,000/= |
| Zaidi ya 65 | A5 | Tsh 150,000/= |

NB:
Gharama hizi zinajumuisha gharama ya maombi ya Leseni Tsh 10,000/=.

www.latra.go.tz 0800 11 00 19 0800 11 00 20



## GHARAMA ZA LESENI

Magari ya Mizigo kwa mwaka

| Uzito (kg) | Leseni | Gharama |
|---|---|---|
| 0 - 999 | C1 | Tsh 20,000/= |
| 1,000 - 4,999 | C2 | Tsh 30,000/= |
| 5,000 - 9,999 | C3 | Tsh 55,000/= |
| 10,000 - 14,999 | C4 | Tsh 60,000/= |
| 15,000 - 19,999 | C5 | Tsh 85,000/= |
| 20,000 - 24,999 | C6 | Tsh 100,000/= |
| 25,000 - 29,999 | C7 | Tsh 120,000/= |
| Zaidi ya Tani 30 | C8 | Tsh 130,000/= |

NB:
Gharama hizi zinajumuisha gharama ya maombi ya Leseni Tsh 10,000/=.

www.latra.go.tz 0800 11 00 19 0800 11 00 20



## GHARAMA ZA LESENI

Mabasi ya masafa marefu kwa mwaka

| Daraja | Gharama |
|---|---|
| Kawaida (Ordinary) | Tsh 120,000/= |
| Kati 1 (Lower Semi Luxury) | Tsh 120,000/= |
| Kati 2 (Upper Semi Luxury) | Tsh 170,000/= |
| Starehe (Luxury) | Tsh 170,000/= |

NB:
Gharama hizi zinajumuisha gharama ya maombi ya Leseni Tsh 10,000/= na gharama ya **Ratiba** Tsh 10,000/=.

www.latra.go.tz 0800 11 00 19 0800 11 00 20




## GHARAMA ZA LESENI

Magari ya Watalii kwa mwaka

| Idadi ya Abiria | Gharama |
|---|---|
| 1 - 15 | $60 |
| 16 - 25 | $90 |
| 26 - 45 | $155 |
| 46 - 65 | $160 |
| Zaidi ya 65 | $170 |

NB:
Gharama hizi zinajumuisha gharama ya maombi ya Leseni **$10**.

www.latra.go.tz 0800 11 00 19 0800 11 00 20



## GHARAMA ZA LESENI

Magari ya Shule (School Bus) kwa mwaka

| Idadi ya Abiria | Gharama |
|---|---|
| 1 - 15 | Tsh 45, 000/= |
| 16 - 25 | Tsh 60,000/= |
| 26 - 45 | Tsh 100,000/= |
| 46 - 65 | Tsh 100,000/= |
| Zaidi ya 65 | Tsh 150,000/= |

NB:
Gharama hizi zinajumuisha gharama ya maombi ya Leseni **Tsh 10,000/=**

www.latra.go.tz 0800 11 00 19 0800 11 00 20



## GHARAMA ZA LESENI

Magari ya wafanyakazi (Staff Bus) kwa mwaka

| Idadi ya Abiria | Gharama |
|---|---|
| 1 - 15 | Tsh 45, 000/= |
| 16 - 25 | Tsh 60,000/= |
| 26 - 45 | Tsh 100,000/= |
| 46 - 65 | Tsh 100,000/= |
| Zaidi ya 65 | Tsh 150,000/= |

NB:
Gharama hizi zinajumuisha gharama ya maombi ya Leseni **Tsh 10,000/=**

www.latra.go.tz 0800 11 00 19 0800 11 00 20

# MHE.MPOGOLO AWATUNUKU VYETI MADEREVA 1,518 WALIOTHIBITISHWA NA LATRA

Mhe. Edward Jonas Mpogolo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala amewatunuku vyeti madereva 1518 waliofanya mtihani na kuthibitishwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na hivyo kufikisha jumla ya madereva 2517 ikiwa ni pamoja na madereva 999 waliothibitishwa hadi Julai 1, 2023.

Mhe. Mpogolo amewatunuku madereva hao katika hafla ya pili ya utoaji vyeti kwa madereva waliothibitishwa na LATRA iliyofanyika Juni 04, 2024 katika ukumbi wa mikutano Arnaoutoglou uliopo Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Mpogolo amewaambia madereva kuwa vyeti walivyotunukiwa vitatambulika kitaifa na kimataifa hasa kwa Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), hivyo ni manufaa makubwa kwa kuwa wanaenda kutanua wigo wa ajira ndani na nje ya nchi hatimaye watajiinua kiuchumi na kijamii.

Vilevile Mhe. Mpogolo amewapongeza madereva hao na amewaeleza kuwa, Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inawathamini na imedhamiria kuongeza hadhi ya madereva na ndio maana kupitia LATRA jambo hilo linafanyika, "Uthibitishaji huu wa madereva utawaheshimisha zaidi na maslahi yenu yataboreshwa na zaidi ya yote, taaluma hii ya udereva itarasimishwa na kukomesha tabia ya baadhi ya wasafirishaji kuwapa kazi ya udereva watu wasiostahili kufanya kazi hiyo."

Kwa upande CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi

>>>Inaendelea Uk. 15



*Mhe. Edward Jonas Mpogolo, Mkuu wa Wilaya ya Ilala akimtunuku cheti moja ya madereva 1518 waliofanya mtihani na kuthibitishwa na LATRA katika hafla iliyofanyika Juni 04, 2024, ukumbi wa mikutano Arnaoutoglou, Dar es Salaam*

>>>Inatoka Uk. 14

# MHE.MPOGOLO AWATUNUKU VYETI MADEREVA....

Mkuu LATRA amewasihi madereva wa vyombo vya moto kibiashara kujitokeza kusajiliwa na kuthibitishwa ili kuongeza thamani katika fani yao ya udereva ukizingatia kuwa suala hilo ni takwa la kisheria na amewasihi kujiendeleza zaidi ili Mamlaka ipate hoja za kurasimisha ajira zao.

Aidha ameeleza kuwa Mamlaka haitatoa leseni kwa basi ambalo halina dereva aliyethibitishwa na LATRA kufikia Julai Mosi, 2024 kwani Mamlaka ilitoa muda wa kutosha kutekeleza Sheria hii, "nawasihi wananchi wasikubali kuendeshwa na madereva wasioweza kufuatiliwa mwenendo wao, kwani wanaposababisha ajali hukimbia na niwasihi wasafirishaji kuwa milango ya kusikiliza wenye changamoto ipo wazi ili msikwame kuendelea kufanya biashara ya usafirishaji."

Vilevile amesema kuwa, madereva waliothibitishwa watapatiwa kitufe cha utambuzi (i-button) chenye taarifa za kila dereva husika, na kitufe hicho ni mali ya dereva, sio mwajiri, na kinapaswa kutumika kila wanapoanza safari na kumaliza safari.

> **"Taaluma hii ya udereva itarasimishwa na kukomesha tabia ya baadhi ya wasafirishaji kuwapa kazi ya udereva watu wasiostahili kufanya kazi hiyo."**
>
> *Mhe. Edward Mpogolo*

CPA Suluo ameongeza kuwa LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani imeandaa video za kuwakumbusha madereva kuhusu masuala ya msingi ya kuzingatia wakiwa barabarani ikiwemo suala la alama na michoro na video hizo zinapatikana LATRA Online TV kwenye mtandao wa YouTube na amewasihi madereva kujielimisha zaidi hata kama wameshapata cheti cha kuthibitishwa.

Akizungumza kwa niaba ya Dkt. Zainab Rashid, Mwenyekiti wa Kamati ya Uthibitishaji Madereva LATRA, Bw. Mohamed Mpinga Naibu Kamishna Mstaafu wa Jeshi la Polisi na Makamu Mwenyekiti wa Uthibitishaji wa Madereva, amewapongeza madereva waliojitokeza kufanya mtihani na kufaulu na anaamini wataenda kutekeleza kwa vitendo barabarani kwa lengo la kupunguza athari za ajali barabarani.

Katika kipindi cha kuanzia tarehe 01 Juni, 2023 hadi 31 Machi, 2024 Mamlaka ilisajili jumla ya madereva 8,729 kwenye kanzidata ya LATRA, ambapo kati yao, madereva 3,254 (sawa na asilimia 37.3) walijitokeza kufanya mitihani na madereva 1,518 wamefaulu na kuthibitishwa na LATRA.



*Wadau mbalimbali wa Usafiri Ardhini wakifuatilia hafla ya pili ya utoaji vyeti kwa madereva 1518 waliothibitishwa na LATRA iliyofanyika Juni 04, 2024 katika ukumbi wa mikutano Arnaoutoglou uliopo Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam.*

# DCP KAHATANO AFAFANUA UPOTOSHAJI KUHUSU TOZO, UDHIBITI WA PIKIPIKI NA MABASI YA SHULE

Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) DCP Johansen Kahatano ametoa ufafanuzi wa taarifa za upotoshaji zinazosambaa mitandaoni kuhusu ulipaji wa tozo kwa mabasi ya masafa marefu, udhibiti wa pikipiki za magurudumu mawili (bodaboda), magurudumu matatu (bajaji), pamoja na mabasi ya shule.



Akizungumza ofisini kwake Dar es Salaam Mei 08, 2024, DCP Kahatano amesema kuwa, Mamlaka inadhibiti bodaboda na bajaji, kwa kutumia Kanuni za Vyombo vya Kukodi za mwaka 2020 iliyotolewa kupitia Tangazo la Serikali Namba 78, ambapo Mamlaka inatoza ada ya TZS. 15, 000/= kwa bodaboda na TZS. 2,000/= ni gharama za maombi kwa hiyo jumla inakuwa TZS. 17, 000/= na bajaji ada yake ni TZS. 20,000/= na gharama za maombi ni TZS. 2,000/= na jumla inakuwa TZS. 22,000/=. "Viwango hivi vilipunguzwa mwaka 2020, kabla ya hapo ada ya bodaboda ilikuwa TZS. 20,000/= badala ya TZS. 15,000/= ya sasa na bajaji ilikuwa TZS. 30,000/= badala ya TZS. 20,000/= ya sasa."

Vilevile amesema Kanuni hizo zilifanyiwa marejeo mwaka 2023 kwa ajili ya kuruhusu mawakala kutoa leseni, kabla ya hapo Mamlaka ilikuwa ikifanya kazi na Halmashauri ambapo waliingia mkataba wa makubaliano na walikuwa wakipanga vituo na kutoa leseni. Kwa sasa Mamlaka imeongeza wigo na inataka huduma hizo zitolewe na mawakala ambao wanaweza kuwa ni Taasisi za Serikali, Vyama vya Ushirika, Makampuni Binafsi au Mtu Binafsi.

Aidha, kwenye udhibiti wa mabasi ya masafa marefu, DCP Kahatano amefafanua kuwa, Mamlaka inatekeleza kwa mujibu wa Kanuni za Leseni za Usafirishaji ya Mabasi ya Abiria ya mwaka 2020 na moja ya mashatri ya Kanuni hizo ni watoa huduma kutakiwa kulipa levi. "Hii inatokana na kifungu cha 35 cha Sheria ya LATRA inayomtaka mtoa huduma kulipa walau asilimia 1 ya mapato ghafi kwa ajili ya levi, suala hili imefafanuliwa zaidi katika Kanuni za Tozo zilizoweka kiwango cha levi cha asilimia 0.5 na utaratibu wa kulipa levi upo kwa wadhibiti wote."

Vilevile DCP Kahatano, ameelezea udhibiti wa mabasi ya shule na amesema kuwa Mamlaka inatoa leseni za mabasi hayo na imeainisha mapungufu yaliyopo kwenye eneo hilo na iliwasilisha mapendekezo yao kwa Shirika la Viwango (TBS) ya kuandaa viwango vya mabasi hayo na mchakato huo unaendelea.

"Wakati tunasubiri viwango, tupo kwenye mchakato wa kurekebisha Kanuni zetu kwa kuweka

>>>Inaendelea Uk. 17

>>>Inatoka Uk. 16

## DCP KAHATANO AFAFANUA UPOTOSHAJI KUHUSU TOZO...

hitaji la mabasi ya shule kukaguliwa mara mbili kwa mwaka ili tuwe na uhakika kuwa watoto wetu wanasafirishwa kwenye mabasi ambayo ni salama. Bado tunaendelea na ufuatiliaji wa kawaida wa mabasi haya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ili kuhakikisha kuwa mabasi yanakuwa katika hali nzuri. Tunaamini huko mbeleni tutakuwa na mabasi yenye viwango na salama zaidi kwa watoto wetu ikiwemo kuwa na camera ndani ya mabasi

# MHA. MBALAWA: MAKOSA YA KIBINADAMU CHANZO CHA AJALI ZA TRENI DUNIANI KOTE

Mha. Hanya Mbawala, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Reli kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amesema kuwa, chanzo cha ajali nyingi za treni duniani kote husababishwa na makosa ya kibinadamu ambayo hufanywa kwa kukusudiwa ama kwa kutokukusudiwa na wafanyakazi mahsusi wa reli (Safety Critical workers).

Mha. Mbawala amebainisha hayo wakati akitoa mafunzo kuhusu makosa ya kibinadamu kwa wafanyakazi mahsusi wa reli kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC) kituo cha Tanga katika mafunzo ya siku moja yaliyoandaliwa na LATRA, Mei 28, 2024.

Aidha, Mha. Mbawala amewaeleza wafanyakazi hao umuhimu wa kuepuka makosa ya kibinadamu kwa sababu nchi hutumia gharama kubwa kununua treni na kujenga miundombinu ya reli, hii itasaidia kupunguza hasara kwa nchi ikiwemo ajali za treni ambazo huharibu miundombinu ya reli na treni yenyewe.

"Mafunzo haya yatasaidia sana katika kuondoa makosa ya kibinadamu miongoni mwenu kwani makosa hayo husababisha hasara nyingi na kubwa kwa taifa ikiwemo ajali za treni ambazo huharibu

>>>Inaendelea Uk. 18



*Mha. Hanya Mbawala, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Reli kutoka LATRA akitoa mafunzo kuhusu makosa ya kibinadamu kwa wafanyakazi mahsusi wa reli kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC) kituo cha Tanga Mei 28, 2024.*

>>>Inatoka Uk. 17

## MHA. MBALAWA: MAKOSA YA KIBINADAMU CHANZO CHA AJALI ZA TRENI...

miundombinu ya reli na treni yenyewe lakini pia kuepuka kupata harasa za mali na hata kupoteza maisha kwa abiria wanaotumia vyombo hivyo," amesema Mha. Mbawala.

Vilevile, ameeleza matarajio ya Mamlaka baada ya mafunzo hayo kuwa ni pamoja na kupunguza makosa ya kibinadamu kama kutotengeneza njia ya treni kwa usahihi na kutofikisha treni ikiwa salama, "tunaamini kuwa wafanyakazi hawa watakua wamezingatia mafunzo tuliyowapatia katika semina hii na sasa hivi tunaamini kabisa makosa ya kibinadamu yatapungua kwa upande wa wafanyakazi hawa, na hii itaboresha huduma za treni nchini na kukuza sekta ya Usafiri Ardhini."

Naye Bw. Rolence Semanini, Meneja wa Reli TRC Kanda ya Tanga amesema, "niwashukuru LATRA kwa kutupatia elimu hii nzuri kwani wametuelekeza mambo ambayo ni msingi mkuu wa usalama wa reli na mambo hayo tunakutana nayo kila iitwapo leo tunapokuwa tukitekeleza majukumu yetu, lakini pia mafunzo haya yameakisi kwa kiasi kikubwa sana utendaji kazi wetu kwa sababu yamegusa idara zote muhimu za uendeshaji wa reli kuanzia utawala hadi watendaji ndani ya treni wakiwemo waongozaji treni na madereva wa treni."

Kwa upande wao, washiriki wa mafunzo hayo wameishukuru LATRA kwa kuwapatia mafunzo hayo kwani yamewapatia mwanga na kuwafanya wawe tayari zaidi kuitumikia sekta ya reli na taifa kwa jumla ili kuleta maendeleo ya pamoja katika

## LATRA KUONGEZA WIGO WA UDHIBITI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeaswa kuongeza wigo wa udhibiti mwenendo wa magari mbali na mabasi ya masafa marefu ili kudhibiti mwenendo usiofaa wa madereva hali itakayoweza kupunguza ajali za barabarani.

Wito huu umetolewa na Mhe. Augustine Holle (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) aliyemuwakilisha Mhe. Deus Sangu (Mb) Mwenyekiti wa Kamati, baada ya ziara iliyofanyika Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Adhini (LATRA) na kukagua shughuli za udhibiti zinazofanywa na Mamlaka ikiwemo ufuatiliaji wa mwenendo wa magari yawapo safarini na uthibitishaji wa madereva, Februari 26, 2024.

> **"Nishauri LATRA mfike hadi kwenye magari mengine tofauti na mabasi ya masafa marefu kama vile magari ya serikali na binafsi ili kupunguza kabisa ajali**
>
> *Mhe. Augustine Holle (Mb)*

Akizungumza baada ya ziara hiyo Mhe. Holle amesema kuwa kutokana na kazi kubwa inayofanywa na LATRA katika kudhibiti ajali, ni wakati wa LATRA kuanza kutumia mifumo yao kudhibiti na magari mengine ili kudhibiti ajali na mwenendo usiofaa wa madereva.

"Tumepita na kuangalia namna mnavyodhibiti ajali kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na kizuri zaidi tumeona kuwa mfumo huu haufuatilii mwendokasi pekee, tumeona kuwa unaweza hata kuonesha endapo gari litasimama mahali kwa muda mrefu bila sababu ya msingi, nishauri LATRA mfike hadi kwenye magari mengine tofauti na mabasi ya masafa marefu kama vile magari ya serikali

>>>Inaendelea Uk. 19



*CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA akiuelezea Mfumo wa Kufuatilia mwenendo wa Magari (VTS) kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) ilipotembelea Ofisi za LATRA Dar es Salaam, Februari 26, 2024.*

>>>Inatoka Uk. 18

# LATRA KUONGEZA WIGO WA UDHIBITI

na binafsi ili kupunguza kabisa ajali," amesema Mhe. Holle.

Aidha, Mhe. Holle ameipongeza Mamlaka kwa kazi kubwa na nzuri inayoifanya ambayo kwa kiasi kikubwa umewezesha kuwepo kwa uwiano mzuri baina ya wasafirishaji na abiria huku akisisitiza umuhimu wa Mamlaka kubadilika kulingana na eneo husika la kiudhibiti.

Kwa upande wake Prof. Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA amewashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ziara na maoni yao huku akielezea utayari wa Mamlaka kuelekea kufanikisha udhibiti wa mwenendo wa magari kwa magari mengine tofauti na mabasi ya masafa marefu.

"Suala la kudhibiti mwenendo wa magari mengine tofauti na mabasi ya masafa marefu Mamlaka imeshalifikiria na kwa kuanzia tuu magari yetu yote yameunganishwa na mfumo huu, kilichobaki ni kuuboresha mfumo ili uwe na uwezo wa kupakia taarifa za magari mengi zaidi na hili linaendelea, nitumie fursa hii kuwashukuru sana kwa kufika LATRA, mbali na kujionea shughuli zetu pia mmetupa maoni mazuri ya kuboresha huduma zetu zaidi, tumeyapokea na tutafanyia kazi," amesema Prof. Ame.

Ili kupunguza ajali za barabarani, Mamlaka ilibuni Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS), huu ni mfumo wa kielektroni unaotumia Satelaiti ili kutoa taarifa za hali ya uendeshaji wa gari husika, taarifa zinazotolewa na mfumo huu ni pamoja na mwendokasi wa gari, kubadili njia (ruti), hali ya ajali na nyingine nyingi.

Kutokana na mfumo huu Mamlaka imefanikiwa kupunguza zaidi ya robo tatu ya ajali ambazo zilikuwa zikitokea nchini pamoja na madhara ambayo yalikuwa yakisababishwa na ajali, mpaka sasa zaidi ya mabasi 7,000 yameunganishwa na Mfumo huu, huku madereva

# WAMILIKI WA KAMPUNI YA MABASI YA SAULI NA NEWFORCE WATAKIWA KUJIELEZA




*DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara kutoka LATRA akizungumza na wawakilishi wa makampuni Newforce na Sauli pamoja na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani katika kikao cha kujadili Udhibiti Usalama wa Usafiri Ardhini Aprili 2, 2024*

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri ardhini (LATRA) imewataka wamiliki wa mabasi ya Sauli na New Force kutoa maelezo kwa maandishi kabla ya kuchukua hatua za kiudhibiti juu yao kufuatia ajali iliyohusisha basi lenye namba ya usajili T175DZU ya kampuni ya New Force na basi lenye usajili T668 DTF Scania mali ya Mwalabhila Sauli Machi 28, 2024 Wilayani Kibaha Mkoa wa Pwani.

Amesema hayo DCP Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabara wakati wa kikao kilichohusisha LATRA, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani pamoja na wawakilishi kutoka mabasi ya Sauli na Newforce Aprili 2, 2024 katika ukumbi wa mikutano ofisi za LATRA Mkoa wa Dar es Salaam.

“Tumebaini kuwa ajali imetokana na uzembe wa madereva na kuwa hakuna usimamizi mzuri wa kampuni hizi katika kutekeleza masharti ya leseni ya usafirishaji. Hivyo kufuatia kikao hiki kampuni hizi ziwasilishe maelezo kwa maandishi kabla ya kuchukua hatua za kiudhibiti dhidi yao,” amesema DCP Kahatano.

Vilevile amesema kuwa kwa mujibu wa taarifa ya Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) Mamlaka imebaini kuwa madereva waliokuwa wakiendesha mabasi hayo kwa siku hiyo hawakutumia kitufe cha utambulisho (i - Button) kabla ya kuanza safari jambo ambalo ni kinyume na masharti ya leseni zao.

Naye ACP. Michael Deleli, Mkuu wa dawati la elimu ya Usalama Barabrani Tanzania amewakumbusha wasafirishaji kutekeleza majukumu yao na utendaji katika kuwasimamia madereva.

“Sisi kama Jeshi la Polisi tunawakumbusha wamiliki wa kampuni za usafirishaji kutekeleza vyema majukumu yenu kwa kuwafuatilia madereva kwa ukaribu pamoja na kutafuta madereva wanaojitambua wawapo barabarani,” amesema ACP Deleli.

Ameongeza kuwa baadhi ya madereva wamekuwa wakikutwa na vimiminika vyenye ulevi jambo ambalo ni kinyume na Sheria na amewasihi kuacha uzembe barabarani ili kunusuru maisha ya Watanzania na mali zao.

Kwa upande wao wawakilishi kutoka mabasi ya Newforce na Sauli wamekiri kuwa ajali iliyotokea imesababishwa na uzembe wa madereva wao na wamejipanga kuendelea kutoa elimu kwa madereva hao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi ili kuhakikisha Usalama wa abiria na mali zao

# CPA SULUO: PUUZENI NAULI ZA SGR ZISIZOTANGAZWA NA LATRA

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewatoa hofu wananchi na amewaasa kupuuza taarifa za nauli za usafiri wa reli ya Kisasa (SGR) zinazosambaa mtandaoni kwa kuwa hazijatolewa na Mamlaka.

CPA Suluo amesema hayo Aprili 24, 2024 ofisini kwake mara baada ya kuona taarifa hizo mitandaoni na ameeleza kuwa hizo ni nauli za awali zinazopendekezwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) ili kuanza kutumika katika usafiri wa reli ya Kisasa (SGR)

“Sisi ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, ni jukumu letu kupanga nauli baada ya kupata maombi kutoka TRC, napenda niwatoe hofu watanzania kuwa wanaosambaza taarifa hizo hatujajua nia yao ni nini, kwanza sio taarifa sahihi na niwahakikishie watanzania kwamba Serikali ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, inawajali watanzania wa aina zote na hasa wale wa hali ya chini, haitoweza kupanga nauli hizi zilizosambazwa katika mitandao ya kijamii, hivyo tunaomba ipuuzwe,” amesisitiza CPA Suluo.

Ameongeza kuwa, pamoja na kutoa nauli, LATRA ina jukumu kubwa la kutoa ithibati ya miundombinu ya reli itakayotumika, pia kutoa ithibati ya mabehewa yatakayokuwa yanabeba abiria.

“Kabla ya kutangaza nauli, lazima tutoe ithibati ya kuanza kutumika kwa njia ya reli na mabehewa. Sio muda mrefu tunatangaza, majaribio yanaendelea na kwa sasa hivi abiria wanaosafiri ni kwa ajili ya majaribio tu, hakuna nauli inayotozwa mpaka Mamlaka itangaze, kwa hiyo ipuuzeni taarifa hiyo na kila mtu aendelee na shughuli zake na hatujui waliotangaza taarifa hiyo wana nia gani,” amesema



*Wajumbe wa Bodi ya LATRA waliongozwa na Prof. Ahmed Ame, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Menejimenti na wafanyakazi wa LATRA wakiongozwa na CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA wakikagua miundombinu ya Reli wakati wa ziara ya Bodi ya LATRA katika mradi wa Reli ya kisasa (SGR)*

# WATOA HUDUMA ZA MIFUMO YA TIKETI MTANDAO WATAKIWA KUJISALI NA MFUMO WA TRA EFDMS KABLA YA MEI, 2024

CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amesema Mei 31, 2024 ndio muda wa mwisho kwa watoa huduma za Mfumo wa Tiketi Mtandao kuunganisha mifumo yao na Mfumo wa Usimamizi wa Mashine za Risiti za Kielektroni (EFDMS) wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mifumo ya Tiketi Mtandao wa Mabasi ambayo haitaunganishwa na mfumo wa TRA EFDMS ili kukidhi hitaji la kisheria la matumizi ya EFD kwa wafanyabiashara ya usafirishaji abiria haitaruhusiwa kutumika kuanzia tarehe 15 Juni, 2024.

CPA Suluo amesema hayo kwenye kikao kilichoshirikisha wadau wa huduma za Tiketi Mtandao, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) katika ukumbi wa mikutano wa LATRA Mkoa wa Dar es Salaam Aprili 30, 2024.

"Kwa Mamlaka tuliyonayo kwa mujibu wa Sheria, na kwa kuzingatia kuwa tumekuwa tukiwapa muda wa kutosha kwenye maandalizi ya kuunganisha mifumo yenu TRA, LATRA inatoa muda wa mwisho kwa anayetaka kusajiliwa kuwa baada ya tarehe 31 Mei, 2024, LATRA itaanza usajili wa watoa huduma waliokidhi takwa la kuunganishwa na TRA EFDMS kwa kipindi cha wiki mbili hadi kufikia tarehe 15 Juni, 2024," amesema CPA Suluo.

Pia, amewakumbusha wamiliki kuwasiliana na timu ya ufundi ya TRA kupitia anwani ya baruapepe efdms.technical@tra.go.tz ili kupata msaada, miongozo pamoja na kukaguliwa kazi zao pindi wanapofanya marekebisho na hatimaye kupata uthibitisho wa TRA na kisha kusajiliwa LATRA kuwa mtoa huduma halali wa Tiketi Mtandao kwa mabasi nchini.

Kuhusu utaratibu wa kuunganishwa na Mfumo

>>>Inaendelea Uk. 23



*Wadau wa huduma za Tiketi Mtandao, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) katika kikao cha kujadili maendeleo ya matumizi ya Tiketi Mtandao, Ofisi za LATRA Dar es Salaam, Aprili 30, 2024*

>>>Inatoka Uk. 22

## WATOA HUDUMA ZA MIFUMO YA TIKETI MTANDAO WATAKIWA KUJISALI......

wa TRA EFDMS, CPA Suluo amesema, Wamiliki wa mabasi au watoa huduma wenye mifumo ya Tiketi Mtandao wanapaswa kuwasilisha maombi TRA ya kufanyiwa majaribio kwa mifumo yao ya Tiketi Mtandao na pale watakapokidhi vigezo vya TRA, watapatiwa Vyeti vya Muunganisho (Certificates & Keys) ambavyo vitawawezesha kuunganisha mifumo yao ya tiketi na ule wa TRA EFDMS katika "Live Environment".

Kwa upande wake Bw. Rodgers Makanyo Makamu Mwenyekiti wa Chama cha watoa huduma za Mifumo ya Tiketi Mtandao amesema watoa huduma za mifumo wako tayari kutekeleza agizo hilo kabla ya Mei 31, 2024 kwani changamoto waliokuwa wanapitia wamezipatia ufumbuzi katika kikao hicho.

Naye Bw. Priscus Joseph, Katibu Mkuu wa TABOA amesema, jambo la kuunganisha mifumo ya Tiketi Mtandao na EFDMS ni jambo jema kwani kuongeza ufanisi wa kulipa kodi za Serikali kutasaidia kuboresha miundombinu inayotumika kutoa huduma hizo ikiwemo

# LATRA YAENDELEA KUBORESHA UDHIBITI WA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI NCHINI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha udhibiti wa huduma za usafiri ardhini nchini ili kuboresha hali ya usafiri na kuchochea maendeleo kwa Taifa.

Hayo yamesemwa na Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi alipowasilisha Bungeni mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Akizungumzia udhibiti wa usalama wa vyombo vya moto kibiashara, Prof. Mbarawa amesema kuwa, Mamlaka imeendelea na usimamizi wa Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) kupitia Kanuni mpya za Matumizi ya VTS ya mwaka 2024 ambazo zimeanza kutumika rasmi Januari 2024.

"Katika kuboresha usimamizi wa VTS, Serikali imeandaa na kutangaza Kanuni za Matumizi ya VTS ya Mwaka 2024 ambazo zilianza kutumika mwezi Januari, 2024 ili kuimarisha Udhibiti na usalama kwa mabasi ya masafa marefu wakati wote kupitia Mfumo wa VTS," amesema Prof. Mbarawa.

Akiongezea kuhusu mfumo wa VTS Prof. Mbarawa amesema, LATRA imeendelea kusimamia na kufuatilia mwenendo wa vyombo vinavyodhibitiwa na kusaidia kupunguza ajali zitokanazo na mwendokasi na kuongeza ufanisi wa vyombo hivyo.

"LATRA imeendelea kufuatilia mwenendo wa mabasi na vichwa vya treni kupitia Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) na hadi kufikia Machi, 2024 mabasi 10, 270 na vichwa 20 vya treni (18- TAZARA na 2 – TRC) vimeunganishwa katika mfumo huo hali iliyosaidia kupunguza ajali kwa asilimia 7.26," amesema Prof. Mbarawa.

> **"Hadi kufikia Machi, 2024 mabasi 10, 270 na vichwa 20 vya treni (18- TAZARA na 2 – TRC) vimeunganishwa katika mfumo wa VTS"**
>
> *Prof. Makame Mbarawa (Mb)*

Vilevile ameeleza kuwa, ili kuwadhibiti madereva, LATRA imeendelea kusajili na kuwathibitisha madereva wa vyombo vinavyodhibitiwa kwa ajili ya kuimarisha usalama wa

>>>Inaendelea Uk. 24

>>>Inatoka Uk. 23

## LATRA YAENDELEA KUBORESHA UDHIBITI WA HUDUMA ZA....

huduma za usafiri ardhini.

"LATRA imeendelea kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vinavyodhibitiwa ili kuboresha ufanisi na usalama, ambapo hadi Machi 2024, Jumla ya madereva 7,867 wamesajiliwa, madereva 1,441 wakiwa wamethibitishwa na LATRA na kati yao 1,190 wamesajiliwa kwenye mfumo wa VTS na kupatiwa vitufe vya utambuzi wa madereva (i-Button)," ameeleza Prof. Mbarawa.

Aidha, Prof. Mbarawa amesema kuwa, Serikali imeiwezesha LATRA kuboresha Mfumo wa tiketi za kielektroni ili kuwawezesha abiria kukata tiketi kwa njia ya mtandao akiwa mahali popote kwa kuanzisha kanuni zinazosimamia mfumo huo.

"Ili kuboresha usimamizi wa tiketi za kielektroni, Serikali imeandaa na kutangaza Kanuni za matumizi ya Tiketi za Kielektroni za mwaka 2024 zilizoanza kutumika Januari, 2024," amesema Prof. Mbarawa.

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inawasihi watumiaji wa vyombo vya moto kibiashara kuendelea kutii Sheria na Kanuni zilizowekwa na Mamlaka

# KIHENZILE AIAGIZA LATRA KURATIBU USHIRIKISHWAJI NA UANDIKISHAJI WA SACCOS KWA VIKUNDI VYA BODABODA NA BAJAJI



*Mhe. David Kihenzile, Naibu Waziri wa Uchukuzi, akijibu swali la Mbunge wa Tarime Mjini Mhe.Michael Mwita Kembaki Februari 14, 2024 wakati wa kipindi cha maswali na majibu Bungeni Jijini Dodoma.*

Mhe. David Kihenzile (Mb), Naibu Waziri Uchukuzi ameiagiza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kuratibu ushirikishwaji na uandikishaji wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kwa madereva wa magurudumu mawili (Bodaboda) na magurudumu matatu (bajaji) nchini kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa usafiri ardhini na kuondoa mivutano baina yao na wasafirishaji wa daladala na mabasi ya abiria.

Mhe. Kihenzile ametoa agizo hilo akijibu swali la Mbunge wa Tarime Mjini Mhe.Michael Mwita Kembaki Februari 14, 2024 wakati wa kipindi cha maswali na majibu Bungeni Jijini Dodoma.

Vilevile ameitaka LATRA kuwaunganisha madereva katika vikundi vya SACCOS ili kuongeza Udhibiti katika sekta ya Usafiri Ardhini.

"Napenda kuchukua nafasi hii kuiagiza LATRA kuongeza Udhibiti wa vyombo hivi kwa kuhakikisha jitihada za kuwaunganisha madereva wa bodaboda na bajaji kupitia SACCOS kwa lengo la kuongeza Udhibiti wao pia niwaombe viongozi mbalimbali wa Serikali nchini kuungana na LATRA kuhakikisha bajaji zinatoa huduma kwa mujibu wa Sheria ili kuepusha madhara ya kiuchumi na kijamii", amesema Mhe. Kihenzile.

Aidha, amewataka madereva bodaboda na bajaji kufuata Kanuni na Sheria kwa kutoingilia huduma za daladala au mabasi ya masafa marefu na kuegesha katika vituo vyao walivyopangiwa huku wakisubiri abiria.

>>>Inaendelea Uk. 25

>>>Inatoka Uk. 24

# KIHENZILE AIAGIZA LATRA KURATIBU USHIRIKISHWAJI

"Kanuni ya 15(h) ya Kanuni za magari ya kukodi inakataza vyombo vinavyodhibitiwa, Kuingilia huduma za daladala au mabasi ya masafa marefu, vilevile LATRA imekua ikikabiliana na changamoto hii ya magari ya kukodi kuegesha katika maeneo ambayo si yao kwa kutoa elimu na kufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha tabia hii inakoma", amesisitiza Mh. Kihenzile.

Kwa upande wake Bw. Johansen Kahatano, Mkurugenzi Udhibiti Usafiri wa Barabrara LATRA ameeleza kuwa, LATRA imeshaanza majaribio ya SACCOS kwa kuanza na Mkoa wa Kilimanjaro na tayari mafunzo yamefanyika mkoani Arusha na inatarajia kuanza mafunzo Mkoani Dodoma.

"Sisi kama Mamlaka tumepokea maagizo kutoka Bungeni na tayari tumeanza majaribio ya SACCOS mkoani Kilimanjaro na tumefanikiwa kufanya mafunzo mkoani Arusha. Tunatarajia muda wowote SACCOS kuanza Mkoani hapo na Februari hii Mamlaka inatarajia kuanza mafunzo Jijini Dodoma, matarajio ni kufanikisha zoezi hili nchi nzima hadi kufikia Mwisho wa mwaka wa fedha 2024", ameeleza Bw. Kahatano.

Vilevile, kupitia SACCOS LATRA imekubaliana na vikundi vya bodaboda na bajaji kuwapatia kazi ya kukata leseni kwa niaba ya Mamlaka na kuwapatia kamisheni kwa ajili ya kazi hiyo ili kuimarisha vyama hivyo na kupata mtaji wa kutosha kuweza kujikimu kiuchumi.

"Kufuatia uboreshaji wa huduma zitolewazo na bodaboda na bajaji sisi kama Mamlaka tumekubaliana zifanye kazi chini ya kivuli cha SACCOS na kupitia huu utaratibu tumekubaliana nao kuwapatia kazi ya kukata leseni kwa niaba ya Mamlaka na kwa kufanya hivyo, watapatiwa kamisheni kulingana na mapato watakayo yakusanya ili kuimarisha vyama vyao na kupata mtaji wa kutosha kujiendeleza shughuli zao za kiuchumi, kupitia hili tunawajengea uwezo wa kujisimamia wao wenyewe", amesema Bw. Kahatano.


Pia Bw. Kahatano ametoa wito kwa madereva bodaboda na bajaji na vyama vya waendesha vyombo hivyo nchini kufikiria muelekeo wa Mamlaka na wajiandae kupokea mabadiliko ya kuimarisha uchumi wao na kuboresha uhusiano wao.

"Nitoe wito kwa vijana na vyama vya madereva bodaboda na bajaji nchini kufikiria muelekeo ambao Mamlaka umekuja nao na waanze kujipanga kupokea mabadiliko ambayo yana lengo la kuwawezesha wao kiuchumi na kuboresha



> **"Pia niwaombe viongozi mbalimbali wa Serikali nchini kuungana na LATRA kuhakikisha bajaji zinatoa huduma kwa mujibu wa Sheria ili kuepusha madhara ya kiuchumi na kijamii**
>
> *Mhe. David Kihenzile (Mb),*

# WAHUDUMU 67 WA MABASI YA MASAFA MAREFU NA MJINI KANDA YA KASKAZINI WAHITIMU MAFUNZO



*Bw. Hadney Chikukuro, Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Arusha akimtunuku cheti mmoja kati ya wahudumu wa mabasi waliohitimu mafunzo yaliyotolewa na LATRA, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) pamoja na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kuanzia Februari 5-9, 2024 katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA)*

Wahudumu 67 wa mabasi ya masafa marefu na mijini Kanda ya Kaskazini Tanzania Bara wamehitimu mafunzo yaliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) pamoja na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kuanzia Februari 5-9, 2024 katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA).

Wahudumu hao wamejifunza masuala mbalimbali ikiwemo Sheria, Kanuni na Taratibu za LATRA, Huduma bora kwa usalama wa abiria na mali, Namna ya kukabiliana na malalamiko ya wateja, Huduma ya kwanza kwa mteja, Utunzaji wa mizigo pamoja na kutambua bidhaa hatarishi, Mfumo wa Tiketi Mtandao, Muitikio wa dharura, Uhusiano na mawasiliano, Unadhifu wa mtoa huduma pamoja na Utunzaji wa mazingira.

Bw. Hadney Chikukuro, Katibu Tawala Msaidizi anayesimamia Uchumi na Rasilimali alimwakilisha Mhe. John Mongella, Mkuu wa Mkoa wa Arusha kwenye hafla ya ufungaji wa mafunzo kwa wahudumu wa mabasi ya masafa marefu na mijini Kanda ya Kaskazini, Tanzania Bara yaliyofanyika katika Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) Februari 9, 2024.

Akisoma hotuba kwa niaba ya Mhe. Mongella, Bw. Chikukuro amewaasa wahudumu hao kutumia maarifa waliyoyapata kwenye mafunzo kwa kufanya kazi kwa bidii, weledi na ufanisi ili kupunguza malalamiko kutoka kwa wateja wao.

"Kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wateja wenu hasa katika namna mnavyowahudumia, ni matumaini yangu kwamba baada ya mafunzo haya mnaenda kubadili utendaji kazi wenu. Pia nawasihi kuyazingatia yote mliyofundishwa na muende kuyatekeleza kwa vitendo ili kuwa na usafiri ardhini ulio na tija," ameeleza Bw. Chikukuro.

Vilevile, ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kuendelea kuleta mabadiliko chanya katika sekta ya usafiri ardhini ikiwa ni pamoja na kuiheshimisha kada ya wahudumu na kuifanya kuwa yenye tija kwa kuwa ni kazi kama kazi nyingine.

Pia, Bw. Chikukuro ametoa wito kwa uongozi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuendelea kuwa wabunifu na kufanya kazi kwa weledi mkubwa ili kukifanya Chuo hicho kuwa mahali sahihi pa kupatia mafunzo stahiki na ametoa rai kwa Chuo hicho kuendelea kutoa mafunzo hayo mara kwa mara ili kuhakikisha wahudumu wanaendelea kutoa huduma

>>>Inaendelea Uk. 27

>>>Inatoka Uk. 26

# WAHUDUMU 67 WA MABASI YA MASAFA MAREFU NA MJINI.......

zinazokidhi vigezo kwa abiria wao.

Naye CPA Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) amewapongeza wahudumu waliohitimu mafunzo na amewaeleza kuwa mafunzo hayo yametolewa kwa mujibu wa Sheria ambapo kwa mujibu wa Kifungu Na 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, Mamlaka ina jukumu la Kusajili Wahudumu na Kuthibitisha Madereva wa vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara.

"Tunawapongeza kwa kuwa ninyi ni wahudumu wa kwanza kupata mafunzo haya na baada ya hapa, tutawapatia vitambulisho vitakavyoonesha kuwa mnatambuliwa na LATRA. Ninawasihi mkaoneshe utofauti mnapotekeleza majukumu yenu na sisi tutawafuatilia ili kuona utekelezaji wa yale mliyofundishwa," ameeleza CPA Suluo.

Kwa upande wake Dkt Zainabu Mshana, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) ameishukuru LATRA kwa ushirikiano na ameahidi kuwa mafunzo hayo yataendelea kutolewa katika Kanda nyingine ili kuwafikia wahudumu wengi nchini.

Vilevile amewasihi wahudumu hao kuwa mabalozi wazuri kwa wahudumu wengine ambao hawakupata nafasi ya kuhudhuria kwenye mafunzo kwa kuwaelekeza masuala muhimu ya kuzingatia pindi wanapotekeleza majukumu yao ili kuifanya sekta ya usafiri ardhini kuwa bora.

Naye Dkt. Cairo Mwaitote amesema mafunzo hayo yataleta chachu katika maendeleo ya sekta ya usafiri ardhini kwa kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wateja.

Akizungumza kwa niaba ya wahitimu wa mafunzo hayo, Bi. Fatma Ally amewashukuru wakufunzi kwa kuwafundisha kwa umahiri na wameahidi



*Mkufunzi kutoka Shirika la Msalaba Mwekundu akiwapatia Wahudumu wa Mabasi elimu ya huduma ya kwanza kwa abiria wawapo safarini, wakati wa mafunzo kwa Wahudumu hao yaliyofanyika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE)*




*Maafisa Usafirishaji waliojitokeza katika hafla ya uzinduzi wa Sare maalum na mfumo wa kidigitali kwa madereva bodaboda na bajaji mkoa wa Dar es Salaam, Julai 1, 2024 katika viwanja vya Mnazi mmoja.*

*Wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhi (LATRA) wakishiriki maandamano ya Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi) Mei 1, 2024 Viwanja vya Uhuru, Jijini Dar es Salaam*





*Wadau mbalimbali waliohudhuria Mkutano wa wadau ili kupokea maoni kuhusu maboresho ya Sheria ya Leseni za Usafirishaji Sura ya 317, Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413 na Kanuni zake, uliofanyika Juni 05, 2024 katika ukumbi wa mikutano wa Arnaoutouglou, Jijini Dar es Salaam.*

**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano cha Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kikiongozwa na Bodi ya Wahariri**

**Mwenyekiti:** CPA HABIBU SULUO | **Mhariri Mkuu:** SAMUEL KEENJA | **Wahariri Wasaidizi:** SALUM PAZZY, MAMBWANA JUMBE | **Waandishi:** MAMBWANA JUMBE, MARIAM NINA, DEUSDEDITY MASEMBA | **Msanifu Picha:** IBRAHIM SAID | **Wapiga Picha:** IBRAHIM SAID, DEUSDEDITY MASEMBA | **Wasanifu Jarida:** IBRAHIM SAID, DEUSDEDITY MASEMBA

**©2024**